

Mchango wa Media za Video katika Ufundishaji wa Kiswahili kwa Wageni

*Arnold B.G. Msigwa
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
agawasike@gmail.com*

Ikisiri

Kujifunza lugha ya kigeni hasa katika kipindi ambacho mjifunzaji akiwa tayari anayo lugha ya kwanza, huambatana na matatizo mbalimbali. Sababu za matatizo haya, mbali na mambo mengine, yanasababishwa na tofauti za kiisimu baina ya lugha ya mjifunzaji na lugha anayojifunza. Pia, hutokana na tofauti za kiutamaduni na kimazingira. Hivyo, ni mchakato ambao wakati fulani hukatisha tamaa miongoni mwa wajifunzaji. Matumizi ya media anuwai vile video katika kufundishia lugha ndiyo suluhu ya matatizo. Kwa hiyo, makala haya yanabainisha mchango wa media za Video katika kufundishia lugha ya kigeni mahususi kwa ajili ya Kiswahili. Aidha, matokeo ya mahojiano yaliyofanywa mwaka 2018 kati ya mwandishi wa makala na wafundishaji wa Kiswahili kwa wageni katika kituo cha MS TCDC¹ (MS Training Center for Development Cooperation) kuhusu matumizi ya video kwa wajifunzaji lugha ya Kiswahili, yanabainisha kuwa video huwasukuma wajifunzaji lugha ya Kiswahili kupenda kujifunza lugha hiyo. Vilevile, video inawapa hamasa (motisha) wajifunzaji wa lugha. Swali linaloibuliwa na makala haya ni: Je, media za kisasa kama vile video zinasaidiaje ujifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni lugha ya kigeni?

1.0 Utangulizi

Makala haya yanafafanua nafasi ya media za video katika kuwezesha umuduji wa lugha kwa wajifunzaji wa lugha ya Kiswahili ikiwa ni lugha ya kigeni. Katika kufafanua vema suala hili, yafuatayo yamemakinikiwa: Mosi, makala yanabainisha usuli kuhusu ufundishaji wa lugha ya kigeni. Pili, makala yamedokeza aina za media zinazoweza kutumika kufundishia lugha ya kigeni, na tatu, makala yanajadili umuhimu wa media za video katika ufundishaji wa lugha ya kigeni, mifano ikidondolewa kutoka lugha ya Kiswahili.

¹ MS inasimama badala ya “Mellempfolkeligt Samvirke” ambalo ni shirika lisilo la kiserikali linalojulikana kama “Danish Association for International Cooperation”

2.0 Usuli wa Ufundishaji Lugha ya Kigeni

Katika taaluma ya Isimu Tumizi kuna mkanganyiko wa watu kuchanganya dhana ya lugha ya pili na lugha ya kigeni. Tunafafanua kidogo dhana hizi mbili ili kutoa uelewa. Lugha ya pili (kuanzia sasa, Lg2) ni ile lugha ambayo mtu hujifunza baada ya kuwa tayari anayo lugha ya kwanza. Aidha, Stern (1983) anafasili Lg2 kuwa, ni ile ambayo mtu anajifunza mbali na lugha yake ya kwanza. Mara nyingi Lg2 hutumika ndani ya nchi au katika mazingira ya mtumiaji. Mathalani, Kiswahili ni Lg2 kwa Watanzania walio wengi kwani kina matumizi mapana. Sifa muhimu za Lg2 ni kwamba huwa inazungumzwa ndani ya nchi ya mjifunzaji lugha huyo. Sifa hii muhimu yaani kutumika ndani ya nchi ya mjifunzaji lugha huyo, ndiyo huitofautisha Lg2 na lugha ya kigeni. Miongoni mwa sifa nyingine za Lg2 ni pamoja na: huwa inakuwa na wazawa wa lugha ndani ya nchi husika na pia huwa na matumizi mapana katika nchi. Kwa kuzingatia sifa hizo zilizotajwa hapa, Kiswahili ni Lg2 ya pili kwa Watanzania wengi hasa wanaozaliwa na kukulia katika mazingira ya vijijini. Hii ni kwa sababu Watazania hawa, huanza kwanza kupata lugha za jamii zao kama vile Kikinga, Kibena au Kihehe ndipo wanajifunza Kiswahili wanapokwenda shuleni.

Kwa upande mwingine, lugha ya kigeni (kuanzia sasa, Lgn) ni ile lugha ambayo mtu hujifunza baada ya kuwa tayari anayo lugha ya kwanza na kuitumia katika mawasiliano fulani fulani; lakini wazungumzaji wake wazawa wako nje ya nchi anakokaa mjifunzaji lugha huyo. Kwa kawaida, lugha ya kigeni huwa haina wazungumzaji wazawa katika nchi ambako wajifunzaji lugha wanajifunza. Kulingana na ufafanuzi huo; Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu na Kichina ni lugha za Kigeni kwa Watanzania wote. Aidha, yafaa kuweka angalizo kidogo hapa kwamba wakati fulani mjifunzaji wa lugha ya kigeni anaweza kutumia mbinu ya uzamaji kindakindaki² ambapo anaamua kuondoka kutoka kwenye nchi yake ya asili na kwenda kujifunzia lugha husika katika nchi ya wazawa. Kwa mfano, Mfaransa, Mwingereza au Mmarekani anasafiri kutoka katika nchi hizo na kuja kujifunzia Kiswahili nchini Tanzania. Lengo lake hasa ni kumwezesha kupata ingizo kamilifu la lugha. Hali hiyo haiondoi ukweli kwamba Kiswahili ni Lgn kwa mjifunzaji lugha huyo. Kitu pekee kilichofanyika ni kubadili mkabala wa kujifunza lugha ya Kiswahili. Kwa hiyo, ni muhimu kutofautisha mkabala wa ujifunzaji ambapo mtu anaweza kujifunza lugha ya kigeni na dhana yenyewe.

2 Mbinu ya Uzamaji Kindakindaki ni tafsiri ya *Total Immersion Approach*. Yaani hali ya mjifunzaji wa lugha ya kigeni kwenda kujifunzia lugha kwa wazungumzaji wazawa wa lugha hiyo.

Awali kabisa lugha iliyoanza kufunzwa kama lugha ya kigeni ilikuwa ni lugha ya Kiakadia³ iliyozungumzwa eneo la Mesopotamia, yaani eneo la Iraq kwa ramani ya leo. Ndiyo lugha ya Kidiplomasia iliyokuwapo kuanzia Milenia ya 3 KK hadi karne ya 8 KK. Utawala wa Akadia ndiyo lilikuwa dola kubwa katika eneo la Mesopotamia. Hivyo, watu wengi walilazimika kujifunza lugha ya Akadia kwa sababu ndiyo lugha iliyotumika katika utawala na kuenezea ustaraabu ikiwamo dini. Wasumeri ndiyo jamii ambayo ilianza kujifunza lugha ya Kiakadia ili kuelewa masuala ya utawala na maarifa yaliyotolewa kwa lugha hiyo. Aidha, upande wa Ulaya, Smith na wenzake (2018) wanabainisha kuwa hadi kufika mwishoni mwa karne ya 16, lugha ya Kilatini ilikuwa ndiyo lugha ya: utawala, taaluma (sayansi), lugha ya biashara na lugha ya kuenezea dini. Hivyo, watu kutoka mataifa tofauti walilazimika kujifunza lugha hiyo ili kupata taaluma anuwai. Baada ya kupoteza nguvu na kuchukuliwa na lugha ya Kiitaliano, Kifaransa na Kiingereza, watu mbalimbali waligeukia katika kujifunza lugha hizo kama lugha za biashara na utawala. MxLelland (2018) anabainisha kuwa kwa kipindi chote hicho hadi kufikia karne ya 18 mbinu za kimapokea kama vile: Tafsiri Sarufi, Mbinu ya Moja kwa moja na Mbinu ya Masikizi ndizo zilizotumika katika kufundishia lugha ya kigeni. Wajifunzaji wa Lgn walijifunza zaidi tafsiri, msamiati mgumu na kukariri sarufi ya lugha lengwa. Mabadiliko katika njia na mbinu za ufundishaji wa Lgn yalianza karne ya 19 na 20 baada ya kuanza kwa isimu tumizi kama taaluma inayojitegemea. Wanaisimu tumizi wa mwanzo ni pamoja na Heinrich Gottfried Ollendorff (1803-1865), Henry Sweet (1845-1912), Otto Jespersen (1860-1943) na Harold Palmer (1877-1949). Katika karne ya 21 kwa kuongozwa na maendeleo ya sayansi na teknolojia, mbinu za ufundishaji wa Lg2 zimebadilika zaidi. Haja ya ushirikishaji wa mjifunzaji Lgn imesababisha kufikiriwa kubadili kwa mbinu ya ufundishaji wa lugha. Kuibuka kwa Mbinu ya Ufundishaji Lugha Kimawasiliano kumebadili njia za kufundishia na kujifunzia lugha. Matumizi ya Media za Video ni miongoni mwa mabadiliko hayo.

Ama kuhusu nadharia ufundishaji Lgn na mwelekeo wa wajifunzaji lugha imebadilika kuanzia miaka 1980 hadi sasa. Mabadiliko haya yamechochewa na mitazamo mbalimbali ya kiisimu, kisaikolojia, kielimu na kisiasa kuhusu ujifunzaji lugha ya kigeni (Hall na Cook, 2012). Aidha, mabadiliko hayo pia yametokana na hali halisi kutokana na ushuhudiaji wa zoezi lenyewe la kufundisha lugha ya

3 Ni tafsiri ya Akkadian language spoken in Far East Akkadian Empire (c. 2334–2154 BC)

kigeni darasani. Hivyo, wafundishaji wa lugha ya kigeni hawana namna ya kukwepa katika kutumia media mbalimbali wakati wa kufundisha lugha kwa wanafunzi wageni. Media ni zana yoyote ambayo mfundishaji wa Lgn anaweza kuitumia ili kurahisisha mchakato wa kujifunza na kufundisha. Media hizi zinaweza kuwa ni za kuona, kusikiliza, kuona na kusikiliza au matini za kusomwa. Wafundishaji wa lugha wamekuwa wakihoji ni kwa vipi media mbalimbali ikiwa ni pamoja na fasihi inavyoweza kutumika kufundishia lugha ya kigeni. Kwa mfano, Babae na Yahya (2014) wanabainisha kuwa ili media zifanikiwe katika kufundishia lugha ya kigeni, mfundishaji sharti azingatie mambo matatu ambayo ni: Mosi, kubainisha lengo la kufundisha lugha akizingatia mahitaji na matarajio ya mjifunzaji. Pili, kuchagua mkabala faafu wa kufundishia ambao utasaidia kufikiwa kwa mahitaji na matarajio ya mjifunzaji, na tatu kuchagua media ambayo inaendana na malengo ya kufundisha lugha. Makala haya kwa hiyo, yanachunguza umuhimu wa Media za Video wakati wa kufundisha lugha ya Kiswahili ikiwa ni lugha ya kigeni. Katika makala haya, video ni picha mwendo inayohusisha mazungumzo, matendo na tajiriba mbalimbali za maisha ya viumbe na vitu katika muktadha fulani.

3.0 Dhana ya Media katika Ufundishaji lugha

Longman (1987) anaonesha etimolojia ya neno media kuwa limetoka katika lugha ya Kilatini *medius* ikiwa na maana ya zana au njia ambazo hutumika kuwasilishia ujumbe kwa kuona au kutamka. Kutokana na fasili hii, media ni zana ya yoyote inayoweza kumika kuwasilishia maarifa au somo darasani. Katika makala haya, media ni kitu chochote chaweza kuwa cha kutazama, kusikiliza au kusoma ambacho walimu wanaofundisha lugha ya kigeni wanaweza kukitumia katika kuwasilisha somo darasani. Kuna media mbalimbali za kisasa ambazo zinaweza kutumika kufundishia lugha ya kigeni na hatimaye kuleta matokeo mazuri kwa mjifunzaji. Kwa ujumla, tunaweza kusema kuwa media za kisasa ni njia za kisasa zinazotumika katika mawasiliano kati ya mwalimu na mwanafunzi katika darasa la kujifunzia lugha ya kigeni. Katika sehemu inayofuata tunabainisha media anuwai zinazoweza kutumika kufundishia Kiswahili kwa wajifunzaji wageni.

4.0 Aina za Media za Kufundishia lugha za Kigeni

Kama ilivyoielezwa katika aya tangulizi kuwa, media ni kitu chochote ambacho kinaweza kutumika kufundishia na kujifunzia lugha ya kigeni. Lengo la kutumia media hiyo ni kurahisisha ujifunzaji wa Lgn. McGrath (2013) anatazama media za kufundishia lugha katika kategoria mbili: Mosi, matini kama maudhui; yaani media huwa ni kichocheo cha mwingiliano wa mawasiliano kati ya mjifunzaji lugha na wanalugha. Pili, media kama lugha, yaani media hulenga mawasiliano kuhusu lugha lengwa. Hivyo, uchaguzi makini wa mifano ya matumizi ni jambo muhimu darasani. Kwa yote mawili, media zinafumbata kategoria zote mbili; yaani hubeba maudhui na kudhihirisha lugha husika ilivyo. Kwa ujumla, tunaweza kusema kuwa media za kufundishia ni kitu chochote ambacho kinaweza kutumika kurahisisha ujifunzaji na ufundishaji wa lugha. Kiisimu media hizi zinaweza kuwa ni za: kuona, kusikiliza, kusoma au kusikiliza na kuona, matendo mbalimbali n.k. Hivyo, media za kufundishia lugha ni nyenzo muhimu katika kuibua ingizo la lugha kwa mjifunzaji kwa njia ya mwingiliano wa lugha na wanalugha kupitia matini zilizomo katika media hizo. Yafaa media hizi ziandaliwe kwa kuzingatia mahitaji ya mjifunzaji lugha na utamaduni husika.

Kuhusu aina za media zinazoweza kutumika kufundishia Lgn, Timoshenko (2015) anazibainisha aina tatu ambazo ni: media za kusikiliza, media za kuona na media za kuona na kusikiliza. Aidha, katika nchi zilizoendelea, ufundishaji wa lugha ya pili au ya kigeni umeambatana na utumiaji wa teknolojia darasani. Ugunduzi wa zana za kileo kama vile: kompyuta, *overhead projector*, kuwapo kwa vifaa vinavyowezesha kuhifadhi picha na sauti (kusikiliza na kuona) na vinginevyo vimesaidia kwa kiasi kikubwa kuongeza fursa za upatikanaji wa umilisi kwa wajifunzaji lugha katika madarasa ya kisasa. Kutokana na maendeleo hayo ya teknolojia, uteuzi wa media za kutumika katika ufundishaji wa lugha ni jambo muhimu. Media hizi zinaweza kuchaguliwa kutoka miongoni mwa hivi vifuatavyo:

- i. Media za kuona na kusikiliza; filamu, katuni, mfululizo wa maigizo, michezo na mahojiano.
- ii. Media zilizopo katika katarasi maalumu: picha, matangazo, kalenda, kadi, magazeti, majarida na matini za kusoma.
- iii. Media zilizomo katika mfumo wa rialia: menu za hotelini, brosha, tiketi za ndege, kadi za harusi, alama za kahawa, kamera na risiti za kununua.

- iv. Media za kusikiliza: habari, mahojiano, matangazo ya moja kwa moja, utabiri wa hali ya hewa na aina mbalimbali za hadithi fupi zinazohusu kazi na dhana ya lugha.

Kwa hakika orodha ni ndefu, kitu muhimu ni kuwa uchaguzi wa media hizi uzingatie muktadha wa darasa na wajifunzaji lugha. Hata hivyo, tukichunguza kwa makini orodha hiyo, tunaweza kugawa katika makundi makuu mawili: Media za maandishi na media za uneni/masikizi. Media za maandishi ni zile ambazo zipo katika mfumo wa maandishi kama vile magazeti, na matini zilizopo katika mfumo wa rialia. Kwa upande mwingine, media za uneni/masikizi ni zile zilizopo katika mfumo wa mazungumzo, kwa mfano, matini za kuona na kusikiliza kama vile filamu, maigizo na michezo mbalimbali. Ianiro (2007) alibainisha media maandishi kuwa ni pamoja na: Ankara za malipo, fomu za kuagiza vitu, maneno yaliyopo katika kioo cha ATM, tovuti, alama za mitaa, kuponi, tiketi za askari wa barabarani, kadi za salamu, kalenda, kadi za taarifa/ripoti, mwongozo wa matumizi ya luninga, nembo za vyakula, magazeti, majarida n.k. wakati matini za uneni ni ujumbe wa simu, matangazo ya redioni, vitabu-mkondoni, filamu, video, programu katika runinga n.k. Media zote hizi, kwa kuzingatia malengo na mahitaji ya wajifunzaji, mwalimu anaweza kuzitumia kufundishia darasani. Nia ya kutumia media hizi ni kuleta uhalisia ndani ya darasa na kumwezesha mjifunzaji wa Lgn kupata ingizo halisi la lugha.

Video zinaingia katika media za kuona na kusikiliza. Video za kufundishia lugha ya kigeni zinaweza kupatikana kutoka kwenye vyanzo mbalimbali kama vile mitandao ya kijamii, kwa mfano, blogu, *Youtube*, *Facebook* n.k. Pia, zinaweza kupatikana kwa mfundishaji mwenyewe kurekodi tukio fulani kwa lengo la kutumia katika kufundishia somo la lugha kwa wanafunzi wageni. Aidha, video zingine zinaweza kupakuliwa kutoka kwenye tovuti rasmi za serikali, mfano tovuti za bunge, wizara na wakala wa serikali. TUKI (2013) wanafasili dhana ya tovuti kuwa ni nafasi katika mtandao wa kompyuta zinapopatikana taarifa mbalimbali. Wanaendelea kueleza zaidi kuwa taarifa hizo zinaweza zikawa zinahusu kazi na biashara. Wakifafanua kuhusu nafasi ya tovuti katika kujifunza lugha ya kigeni, Thorne na Payne (2005) katika utafiti wao kuhusu ujifunzaji wa lugha ya kigeni wanaeleza kwamba tovuti inasaidia katika mwingiliano na mawasiliano kati ya mjifunzaji lugha na lugha lengwa ambapo katika tovuti hizo ndiko video mahususi zenye taarifa mbalimbali kuhusu lugha anayojifunza mwanafunzi hupatikana.

Jukumu la mwalimu ni kuhakikisha kuwa anaweka taarifa muhimu kuhusu lugha hiyo katika tovuti husika ambayo mwanafunzi anaifahamu. Kadhalika, wanaeleza zaidi kwamba video zilizomo katika tovuti zinaweza kutumika katika ufunzaji na ujifunzaji wa lugha ya kigeni kwa kuwasaidia wajifunzaji kujua tamaduni za lugha lengwa. Video zingine zinazoweza kutumika kufundishia lugha wanafunzi wageni ni zile za matukio mubashara.

5.0 Faida za Kutumia Video Kufundishia Lugha ya Kigeni

Media za video zina faida mbalimbali katika kufundisha Kiswahili ikiwa ni lugha ya kigeni, ambazo zinaweza kufafanuliwa kama ifuatavyo:

5.1 Video Inatoa Msukumo kwa Mjifunzaji Lugha ya Kigeni

Video zinapotumika darasani humfanya mjifunzaji wa lugha ya kigeni kushiriki kikamilifu katika zoezi la kujifunza lugha. Bejrami na Ismaili (2016) wanaeleza kuwa kwa siku hizi, video siyo kitu cha kutumika mazingira ya nyumbani, bali ni nyenzo muhimu katika kujifunzia lugha ya kigeni. Hivyo, msukumo huo unatokana na matukio mbalimbali ambayo huambatana na video inayohusika. Allan (1985), kwa mfano, anadokeza kuwa video ni media ambayo ndani yake inahusisha media nyingine ndogondogo ambazo zinaweza kumshawishi na kumfurahisha mwanafunzi pindi anapojifunza lugha ya kigeni. Anataja mfano wa vitu hivyo kuwa ni matukio ya kimichezo na ucheshi katika masimulizi ya hadithi. Hivyo, kutokana na ucheshi huo au michezo iliyomo katika video husika, wajifunzaji wa lugha ya kigeni hupata msukumo wa kuendelea kupenda somo na hatimaye kufikia kilele cha kuelewa lugha anayojifunza. Aidha, mahojiano yaliyofanywa mwaka (2018) kati ya mwandishi wa makala haya na wafundishaji wa Kiswahili kwa wageni katika kituo cha MS TCDC⁴ “*MS Training Center for Development Cooperation* kuhusu matumizi ya video kwa wajifunzaji lugha ya Kiswahili, walikiri wazi kwamba, video nzuri na zenye ucheshi huwasukuma wajifunzaji lugha ya Kiswahili kupenda kujifunza lugha hiyo tofauti na lugha ngeni ikifundishwa pasipo kutumia media ya video. Somo linapofundishwa kwa kutumia zana ya video huwavutia zaidi wanafunzi na kuwa na mantiki. Pia, video inawapa hamasa (motisha) wajifunzaji wa lugha hususani media hizi za video huvutia zaidi zikitumika wakati wa mchana.

4 MS inasimama badala ya “Mellempfolkeligt Samvirke” ambalo ni shirika lisilo la kiserikali linalojulikana kama “Danish Association for International Cooperation”

5.2 Video Inaonesha Uhalisia wa Lugha ya Kigeni Anayojifunza Mjifunzaji

Matumizi ya video katika kufundisha lugha ya Kiswahili ikiwa ni lugha ya kigeni huondoa udhahania miongoni mwa wajifunzaji lugha. Hii ina maana kuwa lugha inayotumiwa na wahusika waliomo katika video hizo, ni halisi. Hivyo, mjifunzaji anapata kujifunza matamshi, mpandoshuko wa mawimbi ya sauti na kiimbo. Akielekea kuthibitisha maelezo haya, Hall (1989), anaeleza kwamba matumizi ya video darasani humwonesha mwanafunzi uhalisia wa kile anachojifunza kwa kusikia na kukiona kwa macho na matendo. Kinachoelezwa katika maelezo haya ni kwamba video huhusisha milango ya fahamu zaidi ya mmoja wakati wa kujifunza. Binadamu hujifunza vitu ikiwa ni pamoja na lugha ya kigeni kwa kutumia milango mitano ya fahamu yaani kusikia, kuona, kuonja, kunusu na kugusa. Matumizi ya video katika kufundishia lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wageni, licha ya kuonesha uhalisi, pia hushirikisha zaidi ya milango ya fahamu zaidi ya mmoja, mathalani kusikia na kuona. Kwa mujibu wa Loneogan (1984) na Stempleski (1991), media ya video inahusisha vielelezo mbalimbali vya kuona na kusikiliza katika darasa la kufunzia lugha ya kigeni mfano ramani na picha, matukio halisi ya watu wakitenda matendo mbalimbali kama kulima, kucheza na kuimba. Hivyo, media hii inaweza kutumika wakati na muda wowote kulingana na mahitaji ya mwalimu.

5.3 Video Zinawasaidia Wanafunzi Kuimarika Stadi Anuwai Mfano Stadi ya Kusikiliza, Stadi ya Msamiati na Stadi ya Mazungumzo

Matumizi ya video katika kufundisha wanafunzi lugha ya Kiswahili ikiwa ni lugha ya kigeni inawasaidia kuimarisha stadi mbalimbali za lugha kwani huwapatia ingizo⁵ la kutosha miongoni mwa wajifunzaji. Mjifunzaji anapoona video, kusikia kinachosemwa na kuona matendo mbalimbali yanayofanywa na wahusika waliomo katika video husika, huongezewa ufahamu mbalimbali kuhusu lugha anayojifunza. Hoja hii inaelekeana na Nadhariatete ya Ingizo ya Krashen (1985) inayoseama kwamba, ili mjifunzaji wa lugha ya kigeni au lugha ya pili aweze kumudu lugha anayojifunza sharti kila siku apate ingizo la kutosha. Hivyo, wajifunzaji wa lugha ya Kiswahili ikiwa ni lugha ya kigeni wanapoangalia video wanapata ujuzi wa stadi ya kusikiliza, pia wanaelewa msamiati ambao haukuwa rafiki na suala hili

5 Ingizo ni fasili ya neno la Kiingereza "Input" katika taaluma ya ujifunzaji wa lugha ya pili ikiwa na maana ni kitu chochote ambacho mjifunzaji wa lugha ya pili/kigeni hukisikia, kukiona, kusoma au kuelekezwa ambacho husaidia kuboresha uwezo wake wa kutumia lugha tofauti na ule aliokuwa nao awali.

linawezesha kujua msamiati mwingi na kuweza kuelewa mazungumzo kutokana na kile walichokiangalia, hivyo, kuwawezesha wajifunzaji hawa kupata ingizo litakaowasaidia kupata ufahamu wa lugha wanayojifunza.

5.4 Hukuza Uelewa wa Utamaduni wa Jamii Inayohusika

Matumizi ya video au sinema katika darasa la wajifunzaji wa lugha ya kigeni huchangia wajifunzaji kuelewa utamaduni wa lugha lengwa wanayojifunza. Kwa kutazama video zinazoonesha matumizi ya Kiswahili, huwaonjesha ladha ya moja kwa moja ya utamaduni wa Kiswahili. Walimu wanapoleta video au sinema katika darasa, na kuonesha matukio mbalimbali ya jamii kwa wanafunzi, kwa kiasi kikubwa wajifunzaji hupata uelewa mkubwa wa utamaduni wa jamii kupitia matukio hayo. Kwa mfano, video inayoonesha jinsi jamii ya Wahaya wanavyoana. Mjifunzaji wa lugha ya pili akiangalia kisa hiki anaelewa utamaduni unaofungamana na suala la ndoa kwa jamii husika. Bejrami na Ismaili (2016) anashadidia hoja hii kwa kueleza kuwa matumizi ya video huchochea uibuzi wa ingizo asilia la kutosha miongoni mwa wajifunzaji wa lugha ya pili au ya kigeni.

5.5 Video Huwafanya Wajifunzaji kuwa Makini

Kufundisha lugha ya Kiswahili ikiwa ni lugha ya kigeni kwa kutumia video kuna faida ambazo njia zingine za ufundishaji hazina. Mlio mzuri wa sauti, mandhari nzuri ioneshwayo pamoja na mwonekano mzuri wa picha una athari chanya kwa wajifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Mwonekano mzuri na sauti laini huwavutia wajifunzaji na kuwa makini wakati wote wakati somo linaendelea. Hali hii haiwachoshi wala kuwakera wajifunzaji wa Kiswahili. Matumizi ya video kwa kiasi kikubwa yanashabihiana na Mkabala wa Upendekezi unaohimiza matumizi ya muziki laini darasani na mazingira mazuri ya kujifunzia. Hivyo, video zenye mvuto, sauti laini huvuta umakini wa wanafunzi. Kwa mujibu wa Wang (2015) hali hii ya umakini wa wajifunzaji itasababisha kuimarika katika ujuzi wao wa kutumia lugha na walimu kuweza kufikia malengo yao ya kufundisha lugha ya kigeni.

5.6 Video ni Chanzo cha Taarifa

Wajifunzaji wa lugha ya Kiswahili ikiwa ni lugha ya kigeni wakitazama video au sinema hupata taarifa nyingi kwa wakati mmoja. Taarifa hizi zinaweza kuwasaidia wajifunzaji wa lugha ya Kiswahili ikiwa ni lugha ya kigeni kupata ingizo la kutosha

kwa wakati mmoja. Hujifunza mila na desturi katika video, husikiliza, huona mazingira halisi ambamo matendo na matukio ya wahusika hufanywa. Kwa mujibu wa Oddone (2011) matumizi ya video kwa wajifunzaji wa kiwango cha juu, video huongeza taarifa za ziada zaidi kuliko wajifunzaji wa lugha wa viwango vingine kama kile kiwango cha awali au kiwango cha kati. Sababu inayofanywa wajifunzaji wa kiwango cha juu kuongeza taarifa zaidi za ziada ni kutokana na kwamba wanafunzi hao uwezo wao wa kutumia lugha ni mkubwa na hivyo uelewaji wa maana na ishara mbalimbali zinazoweza kuonekana katika video hizo ni mkubwa tofauti na wa viwango vingine. Hivyo, video ni media muhimu katika kufundisha Kiswahili ikiwa ni lugha ya kigeni.

5.7 Video Huwashughulisha Wajifunzaji

Kulingana na Bejrami na Ismaili (2016) baadhi ya walimu na wafundishaji wa lugha za kigeni huona kuwa matumizi ya video darasani ni kwa ajili ya burudani na starehe zaidi kuliko kujifunza. Imedokezwa katika sehemu ya 4.0 kuwa media za kufundishia lugha zinaweza kutazamwa kwa namna mbili: media kama maudhui; yaani media huwa ni kichocheo cha mwingiliano wa mawasiliano kati ya mjifunzaji lugha na wanalugha. Pili, media kama lugha, yaani media hulenga mawasiliano kuhusu lugha lengwa. Kwa hiyo, video kama media ya mawasiliano huwafanya wajifunzaji wa somo muda wote kushiriki katika kufuatilia kile kinachooneshwa katika video husika. Hali hii huendelea kuwafanya wajifunzaji kushiriki katika somo husika pasipo kuchoka. Kwa kufanya hivyo, wajifunzaji hufuatilia matendo na mazungumzo yanayofanywa na wahusika katika video. Njia hii ya video ni nzuri kutumika wakati wajifunzaji wakiwa wamechoka hasa madarasa ya mchana baada ya kula na yale ya jioni.

6.0 Mambo ya Kuzingatia katika Matumizi ya Video

Katika suala la elimu na ufundishaji darasani, lazima mwalimu awasimamie wanafunzi wake ili kuhakikisha kwamba ujifunzaji bora unafanyika. Ufundishaji wa lugha ya Kiswahili kwa njia ya video hauna tofauti na ufundishaji mwingine, hivyo, mwalimu hana budi kuwasimamia wanafunzi wake kwa kupanga jinsi ya kutumia hizo video na aina ya video atakazozitumia. Katika kutumia video katika darasa la wanafunzi wageni, mwalimu afanye mambo yafuatayo:

6.1 Uchaguzi wa Videoa za Kutumia

Mwalimu achugue video kwa kuzingatia maudhui yaliyomo katika video husika. Ili maudhui hayo yawe na maana kwa wajifunzaji, lazima mwalimu apitie hiyo video kabla ya kuipeleka darasani ili kutambua matamshi yaliyomo na usahihi wake. Katika matamshi, ataangalia matumizi ya mkazo kama yako sahihi, ufasaha wake kwa kuzingatia lugha ya Kiswahili. Ama kuhusu msamiati uliotumika humo, ataangalia ugumu au wepesi kwa kuzingatia viwango vya wajifunzaji. Kwa mujibu wa Wang (2015), video ambazo ni ngumu kueleweka kwa wajifunzaji hazina msaada kwa wanafunzi wageni, badala yake ni kikwazo. Lengo la kufundisha lugha ya kigeni kwa kutumia video siyo kuleta utata au ugumu wowote ule, bali ni: mosi ni kukuza uwezo wa kusikiliza wa lugha ya kigeni; pili, kukuza umilisi wa lugha na utamaduni ili kuweza kuwasiliana, na tatu, kuwawezesha wajifunzaji kutambua na kuthamini mchango wa video katika kujifunza lugha wajifunzayo. Hivyo, mwalimu kabla ya kuruhusu video kupelekwa darasani anatakiwa kuipitia na kukagua kwa kuzingatia kiwango cha wanafunzi wanaotarajia kutazama video hiyo ili kuona ikiwa malengo hayo yatafikiwa.

6.2 Aina ya Madarasa

Haya yanarejelea aina ya wanafunzi ambao watakwenda kufundishiwa hiyo video. Muandaaji wa media ya video hana budi kuangalia umri wa wajifunzaji, uwezo wao walionao kuhusu lugha. Pia, azingatie daraja la wajifunzaji lugha ambao anatarajia kwenda kuitumia hiyo teknolojia, yaani ikiwa ni daraja la chini, kati na juu ili kujua mtindo upi wauweke kwenye media ili kufundishia lugha lengwa ya kigeni.

6.3 Ukubwa wa Darasa

Kuhusu ukubwa wa darasa, kinachorejelewa hapa ni idadi ya wajifunzaji. Chapelle (2001) anaeleza kwamba kabla ya uandaaji wa media za video, mwalimu hana budi kuzingatia idadi ya wanafunzi kama kubwa, ndogo au ya kati. Idadi ya wanafunzi inaweza kuathiri uthabiti wa matumizi ya video hiyo, yaani kuonekana kwa kila mwanafunzi au kusikika kwa kila mjifunzaji. Video iwe na sauti ambayo kila mtu atakuwa na uwezo wa kusikiliza na kuelewa kinachosemwa bila tabu yoyote. Video iweze kuonekana kwa kila mjifunzaji kwa namna isiyotia mashaka kwa yeyote, mathalani, sauti ndogo, kutoonekana vizuri kwa video kwa wanafunzi walio mbali au nyuma, hivyo, kupata stadi ya kusikiliza pekee ambayo inahusisha mlango wa

fahamu moja tu. Ni vizuri katika ujifunzaji kutumia milango ya fahamu walau zaidi ya mmoja, kwa mfano, masikio na macho.

7.0 Hitimisho

Media za video zinajumuisha taarifa mbalimbali kuhusu jamii na utamaduni wa lugha ya Kiswahili. Media za video, haziwapi wajifunzaji uhalisia tu wa lugha ya Kiswahili na mazingira ambamo mawasiliano kwa kutumia lugha hufanyika, lakini pia zinawajengea uwezo wa kutambua na kuthamini nafasi ya video katika kujifunza. Ni mbinu shirikishi na huchangamsha darasa. Hivyo, walimu lazima wawe na lengo bayana katika ufahamu wao wa kutumia video mahususi na mikakati ambayo wataitumia ili video ziweze kukuza ufahamu wa wajifunzaji lugha ya Kiswahili na hatimaye kuwapatia ingizo la kiisimu, kiutamaduni na kiufahamu.

Marejeleo

Allan, M. (1985). *Teaching English with Video*. Longman: Harlow, Essex.

Babae, R. & Yahya, W. (2014). Significance of literature in foreign language teaching. *International Education Studies*, 7(4), 80-85.

Barker, J. na Tucker, R. N. (1990). *The Interactive Learning Revolution: Multimedia in Education and Training*. Kogan Page: London.

Bejrami, L na M, Ismaili (2016). International Conference on Teaching and Learning English as an Additional Language, GlobELT 2016, 14-17 April 2016, Antalya, Turkey

Chapelle, C. A. (2001). *Computer Applications in Second Language Acquisition*. CUP: Cambridge.

Hall, G and Cook, G (2012). Own-language Use in Language Teaching and Learning: State of the Art. *Language Teaching* 45/3: 271–308.

Hill, B. (1989). *Making The Most of Video*. London: CILT.

Ianiro, S. (2007). *CALPRO Professional Development Fact Sheet-1: Authentic Materials*. Imepakuliwa kutoka <http://www.calpro-online.org/documents/factsheetauthenticmaterials.pdf>.

- Krashe, S. D (1985). *The Input Hypothesis: Issues and Implications*. Longman Group: UK Ltd.
- McGrath, I. (2013). *Teaching Materials and the Roles of EFL/ESL Teachers: Practice and Theory*. London: Bloomsbury.
- MxLelland, N (2018). The History of Language Learning and Teaching in Britain. Katika *The Language Learning Journal*. Juz. (1), 46. Imepakwiwa Februari 2, 2018.
- Oddone, C (2011). "Using Videos from YouTube and Websites in the CLIL Classroom". Katika *Studies about Languages*. 2011. Na. 18: University of Genoa: Italy.
- Smith, R na wenzake (2018). Histories of Language Learning and Teaching in Europe. Katika *The Language Learning Journal*. Juz. (1), 46. Imepakwiwa Februari 2, 2018.
- Stempleski, S. (1991). "Teaching Communication Skills with Authentic Video". Katika *Video in Second Language Teaching: Using Selecting and Producing Video for The Classroom*, eds. S. Sterompleski and A. Arcario, uk. 7-24. Alexandria, Virginia: TESOL. Inc.
- Stern, H. H. (1983). *Fundamental Concept of Language Teaching*. Oxford: Oxford University Press.
- Timoshenko V. I. (2015). *The use of Mass Media in the English language teaching process*. Karaganda: Chuo Kikuu cha Karaganda.
- Thorne, S. L., & Payne, J. S. (2005). "Evolutionary trajectories, internet mediated expression, and language education". *Jarida la CALICO*, 22, 371-397.
- TUKI, (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.
- Wang, Z (2015) "An Analysis on the Use of Video Materials in College English Teaching in China". Katika *International Journal of English Language Teaching* Juz. 2, Na. 1; 2015: Chuo Kikuu cha Dongbei.